

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA



**TAARIFA KUHUSU MWENENDO WA UGONJWA WA HOMA YA MGUNDA
(LEPTOSPIROSIS) MKOA WA LINDI**

DAR ES SALAAM, 29 JULAI, 2022

Ndugu wananchi; Wizara inapenda kutoa maelezo zaidi kuhusu ugonjwa wa homa ya mgunda (**Leptospirosis**) **ambao** tarehe **18 Julai 2022** tulitoa taarifa kwa umma juu ya uwepo wa ugonjwa huu nchini baada ya uthibitisho wa kimaabara. Taarifa za ufuatiliaji wa ugonjwa huu kutoka kwa wataalam wetu walioko Mkoani Lindi zinaonesha kuwa toka tarehe 18 Julai 2022 hadi sasa **hakujawa na mgonjwa mpya** aliyeonesha dalili za ugonjwa huu. Hivyo hadi kufikia asubuhi ya leo tarehe 29 Julai 2022, idadi ya wagonjwa waliothibitishwa kuugua ugonjwa huu nchini ni **20** na na kati yao 3 wamefariki.

Hivi sasa hakuna mgonjwa aliylazwa wote wameruhusiwa kurudi nyumbani na wanaendelea na shughuli zao. Hii inaendana na sayansi inayojulikana kwa ugonjwa huu kuwa, **ugonjwa huu unatibika kwa kutumia dawa** ambazo zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Aidha, timu ya ufuatiliaji imebaini kuwa, mionganoni mwa watu waliotangamana na wagonjwa hao (contacts) hakuna aliyeonyesha dalili za ugonjwa huu hadi kufikia sasa. Hii inadhibhirisha pia, ni **mara chache ugonjwa huu huambikizwa kutoka binadamu mmoja kwenda kwa mwengine**. Vilevile, wataalamu wetu wanaendelea na utafiti wa kina kwa binadamu, wanyama na mazingira yanayowazunguka ili kubaini na kuweka mikakati ya kuudhibiti ugonjwa huu nchini.

Ndugu wananchi, Maandiko ya kisayansi yanaeleza kuwa, kwa kawaida ugonjwa huu unakuwa na dalili ambazo sio kali kwa asilimia 90, isipokuwa kwa wagonjwa wachache, (asilimia 10), wanaweza kuwa na dalili kali kama kutokwa na damu na kuathirika kwa viungo kama figo, ini n.k. Aidha, **uwezo wa kuuchunguza kwa njia ya maabara upo** hapa nchini, hivyo wananchi wanatakiwa **kutokuwa na hofu**. Ni muhimu wanapokuwa na dalili za ugonjwa huu **kuwahi** kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata **matibabu stahiki na kwa wakati**.

Ndugu wananchi, Napenda kuwakumbusha tena kuwa ugonjwa wa homa ya Mgunda (leptospirosis) huambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kupitia uchafuzi wa mazingira ikiwemo vyanzo vya maji vilivyochofaliwa na mkojo wa wanyama wenye maambukizi. Maambukizi ya ugonjwa huu kwenda kwa binadamu hupitia njia zifuatazo;

- i. Kugusa mkojo (au maji maji mengine ya mwili) kutoka kwa wanyama wenye maambukizi.
- ii. Kugusa maji, udongo, au chakula kilichochafuliwa na mkojo wa wanyama wenye maambukizi.
- iii. Kunywa maji yaliyochafuliwa na vimelea vya bakteria wa ugonjwa huu

Aidha, bakteria wanaweza pia kuingia mwilini kupitia ngozi au utando wa macho, pua au mdomo (*mucous membrane*) na kupitia ngozi yenye mikwaruzo. Maambukizi ya ugonjwa huu kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine hutokea kwa nadra sana.

Ndugu Wananchi, Wizara inaendelea kusisitiza kuwa, wananchi waendelee kuchukua tahadhari zote stahiki za kujikinga na ugonjwa huu ikiwemo kuepuka kutumia maji au vitu vilivyochofaliwa na mkojo wa wanyama pia kunywa maji safi na salama ambayo yamechemshwa au kutibiwa. Wagonjwa wenye dalili za ugonjwa huu ikiwemo **homa, kuumwa kichwa, maumivu ya misuli, uchovu wa mwili, mwili kuwa na rangi ya manjano, macho kuvilia damu, kutoka damu puan, kukohoa damu, kichefuchefu na kuharisha** wahakikishe wanafika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mapema ili wapate uchunguzi na matibabu sahihi. Pia, Wizara inaendelea kuwataka wananchi kutoa taarifa za wagonjwa wanaoonyesha **dalili za ugonjwa** huu zilizoelezwa hapo juu endapo watabainika kuwepo katika maeneo yao.

Mwisho, Wizara inaendelea kuwasistiza wananchi kutokuwa na hofu kwani ugonjwa huu umekwisha dhibitiwa. Vilevile, Serikali ina uwezo wa kuendelea kuchunguza, kutibu na imeweka mikakati ya kuudhibiti ugonjwa huu nchini.

Imetolewa na;


Mhe. Ummy A. Mwalimu (MB)
Waziri wa Afya



Jiandae Kuhesabiwa tarehe 23 Agosti, 2022